

## Relief and Development Services Tanzania- Morogoro Centre

P.O. Box 6123 \* Morogoro \* TANZANIA \* East Africa

### SHULE YA UANAFUNZI



#### **"Kumjua Mungu na kumjulisha kwa wengine"**

Shule ya Uanafunzi (SYU) – Discipleship Training School (DTS) ya Youth With A Mission (YWAM- WAIWAM) ni mfulululizo wa masomo yanayokusudiwa kumuandaa mwamini mkristo mwokovu kuweza kuwa na uwezo mzuri wa Roho Mtakatifu kumshuhudia Yesu katika maneno na mwenendo wake.

#### Kwa ufupi DTS inakazia katika maeneo haya matano:

"Mtumishi na Mungu wake"

"Mtumishi na Neno la Mungu"

"Mtumishi na vita vya kiroho"

"Mtumishi na mahusiano wake na wengine"

"Mtumishi na uinjilisti"

Jumla ya muda wa shule ni wiki 20. wiki 12 darasani (Lecture Phase) na zingine 8 kipindi cha mazoezi (Outreach Phase) sehemu mbalimbali. Kila siku kuna vipindi vya darsa na kazi za mikono na kutoka nje siku moja kila wiki yaani mazoezi (outreach).

#### **Ada ya shule**

Kila mwanfunzi anatarajiwa kulipa ada yake yote siku ya kwanza ya shule. Huduma ya YWAM tunaishi kwa imani na (kumtegemea Mungu kukukatana na mahitaji yetu kupitia ndugu, marafiki, makanisa, mashirika n.k.) hakuna mtu miongoni mwetu anayepokea mshahara. Na Mungu ni mwaminifu kukutana na mahitaji yetu yote.

Ada ya shule ni Tsh. 600,000. Tunaomba urudishe fomu hii pamoja na Tsh.10,000, ada ya kujiandikisha chuoni; haitarudishwa.

Tarehe za shule: Kuanzia \_\_\_\_\_

#### **Makazi, malazi na chakula**

Makazi yetu ni ya wastani tu. Wanafunzi na vijana wafanyakazi wanaishi katika mabweni. Tunayo malazi ya familia. Chakula chetu ni cha mtanzania wa kiwango cha wastani na si cha kifahari.

#### **MUHIMU**

Utakapokuwa umeturudishia sehemu zote za fomu tutakuandikia barua ya kukujulisha kuwa umekubaliwa chuoni au la. Kwa hivyo isipokuwa kwa mawasiliano maalum na wewe au kiongozo wako wa kiroho ngojewa barua hii. Kwa hivyo wasilisha fomu yako mapema kabla ya tarehe za shule.

N.B. Hatapokelewa shuleni kama hujaja na ada yote siku ya kwanza ya shule.

Ukirudisha fomu tunaomba uhakikishe kwamba umetuma kila litu ambacho kimetajwa kwa wakati mmoja. Hatutaweza kuangalia fomu kama hatujapata kila kitu. Tafadhali ujaze fomu hii na kuituma mapema.

#### **YWAM TUNAVYOAMINI**

- o Youth With A Mission au YWAM {inasomeka "waiwam"} ni huduma ya kimadhehebu na kimataifa inayofanya kazi karibu nchi 10 ulimwenguni na ina zaidi ya vituo 900. Lengo ni kuihubiliri injili ulimwenguni katika kizazi chetu na kuwaandaa wengine kwa mafundisho mbalimbali ili waweze kufanya sehemu yao katika kutumikia mwito mkuu katika mathayo 28:19-20
- o Tunaamini katika wokovu wa mtu mzima-roho, mwili na nafsi, vyote vimemtukuza Mungu.
- o Tunaamini neon la Mungu yaani Biblia ndilo lenye mamlaka yote linafundisha kuwa. Yesu ni Mwana wa Mungu na kuwa Yeye tu ndiye mkombozi wa mwanadamu kutoka dhambini,
  - ❖ Katika mamlaka ya wateule kupitia Roho Mtakatifu.
  - ❖ Kiwa Yesu anfanya kazi alizofanya alipo kuwa Duniani kupia wanaomwamini.
  - ❖ Katika mwili mmoja wa Yesu yaani wote wanaomwamini na kumjua kwa kusamehewa dhambi na kutembea katika utakatifu.
  - ❖ Kuwa Yesu atarudi kulichuwa kanisa na kwahivyo ni sharti wote waisikie injili kupitia wote wanao liitia jina la Yesu kwa kweli.